TMA
TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



## JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

*Na.12: Msimu wa Kilimo 2025/26* *Tathmini ya Januari 21 -31, 2026 na Matazamio kwa Kipindi cha Februari 1-10, 2026*

**MUHTASARI**

- Hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki na Pwani ya kaskazini itasaidia zao la mahindi lililo katika hatua ya kukomaa na kukauka.
- Wakulima na wadau wa kilimo wanashauriwa kushirikiana na maafisa ugani katika maeneo yao huku wakiendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa kwa mipango thabiti ya shughuli za kilimo.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 21-31, 2026


Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kupungua nguvu. Hali hii ilipelekea mwenendo wa ukandamvua (ITCZ) kuelekea kusini na kuwepo katika maeneo ya magharibi mwa nchi, nyanda za juu kusini magharibi na kusini mwa nchi.

Kwa upande mwingine joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Afrika mashariki) lilikuwa la chini ya wastani. Hali hii ilipunguza nguvu ya mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki. Hata hivyo, vipindi vichache vya upepo uvumao kutoka baharini viliimarisha mifumo isababishayo mvua nyepesi katika maeneo hayo.

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea uwepo wa vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi, kati, nyanda za juu kusini magharibi na kusini mwa nchi na mvua nyepesi katika maeneo ya ukanda pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki.

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 21-31, 2026

Katika kipindi hiki cha dikadi, baadhi ya maeneo nchini yalipata mvua kati ya milimita 11 hadi 150 kwa siku kumi. Hata hivyo, maeneo machache katika mikoa ya Dodoma (wilaya ya Chemba na Chamwino), Tabora (wilaya ya Igunga na Tabora mjini), Mbeya (wilaya ya Uyole na Chunya), Njombe (wilaya ya Makete, Ludewa na Njombe mjini), Singida (Wilaya ya Manyoni na Iramba magharibi), Rukwa (wilaya ya Mbinga) na Lindi (wilaya ya Nachingwea) yalipata kiasi cha mvua cha zaidi ya milimita 100 kwa siku kumi na maeneo mengi ya mikoa ya Manyara, Arusha , Kilimanjaro, Tanga, Pwani pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba yalikwa makavu kwa ujumla kama inavyoonekana kwenye kielelezo.




Kielelezo 1: Jumla ya mvua kwa siku kumi kwa kipindi cha Januari 21-31, 2026

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 21-31, 2026

Katika dikadi hii, maeneo mengi nchini yalipata mvua ambayo iliongeza unyevu nyevu katika udongo na kusaidia ukuaji na maendeleo ya mazao. Kwa mkoa wa Dodoma, mvua hizi zimesaidia katika ukuaji na maendeleo ya zaola alizeti na mtama. Hata hivyo, kwa mkoa wa Kagera mvua hizi zimeathiri mazao ambayo bado yako mashambani yanasubili kuvunwa.

Kwa maeneo yanayopata mvua za Vuli hususan ukanda wa pwani ya Kaskazini mahindi yalikuwa katika hatua ya kukomaa wakati katika maeneo ya mikoa ya Kagera, Mwanza na Kilimanjaro hususan wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro, wakulima waliendelea na shughuli za uvunaji wa mahindi. Aidha, zao la mpunga liko katika hatua ya ukuaji katika mkoa wa Morogoro. Hata hivyo, hali ya ukavu imeathiri ukuaji na maendeleo ya mahindi katika maeneo ya mengi ya Pwani ya Kaskazini.

Kwa upande wa maeneo yanayopata mvua za Msimu, mahindi yapo kwenye hatua ya ukuaji isipokuwa katika mkoa wa Tabora na Mtwara ambako mahindi yapo katika hatua ya kuota. Hata hivyo, wakulima katika mikoa ya Dodoma waliendelea

na shughuli za upandaji (alizeti na mtama), kutokana na kuchelewa kuanza kwa mvua za Msimu katika maeneo hayo.

Kwa upande wa mazao ya muda mrefu, zao la Kahawa lilikuwa katika hatua ya kutunga tunda hususan katika mikoa ya Kilimanjaro na Songwe.

Maji na malisho kwa ajili ya mifugo na wanyama vimepungua kwa baadhi ya maeneo nchini kutoka na hali ya ukavu iliyokuwepo.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 21-31, 2026

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito kilipungua husussan kwa maeneo ambayo yaliyokuwa na upungufu wa mvua kwa ujumla.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 1-10, 2026

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kuimarika. Hali hii inatarajiwa kuendelea kudumisha mwenendo wa sehemu ya ukandamvua kuelekea kusini na kuwepo katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi yetu, nyanda za juu kusini magharibi na kusini, kanda ya kati na kusini mwa nchi. Aidha, uwepo wa Kimbunga "FYTIA" katika eneo la rasi ya Msumbiji unatarajiwa kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika baadhi ya maeneo ya pwani ya kusini, hususan katika kipindi cha siku tano za mwanzo. Kwa upande mwingine joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Afrika Mashariki) linatarajiwa kuendelea kuwa la chini ya wastani. Hali hii inatarajiwa kudhoofisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani ya kaskazini ya nchi yetu na nyanda za juu kaskazini mashariki.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 1-10, 2026

Maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (mkoa wa Tanga, kaskazini mwa Morogoro na Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), Pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) pamoja na nyanda za juu Kaskazini yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

Maeneo ya kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) yanatarajiwa kuwa na mvua katika maeneo machache.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 1-10, 2026

Hali ya mvua inayotarajiwa nchini itasaidia kuongeza unyevu nyevu katika udongo na kusaidia ukuaji na maendeleo ya mazao. Hata hivyo hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo ya nyanda za juu Kaskazini, Pwani ya Kaskazini pamoja na kanda ya kusini inaweza kuathiri ukuaji na maendeleo ya mahindi ambayo yapo kwenye hatua ya kutoa mbelewele.

**Ushauri:**

- **Maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua (kanda ya ziwa Victoria, Pwani ya Kaskazini na Nyanda za juu Kaskazini Mashariki):** Hali ya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi inayotarajiwa hususan katika maeneo ya kanda ya Ziwa inaweza kuathiri mahindi yaliyo katika hatua ya kukomaa na kukauka **.** Wakulima katika maeneo haya wanashauriwa kuchukua hatua kutokana na hali hii inayotarajiwa.
  Aidha, wanashauriwa kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku kwa mipango thabiti ya shughuli za kilimo.
- **Maeneo yanayopata msimu mmoja wa Mvua (nyanda za juu kusini magharibi, mikoa ya magharibi, Pwani ya kusini na Kanda ya kusini):** Mvua zinazotarajiwa katika maeneo haya zitasaidia ukuaji wa mazao. Wakulima wanashauriwa kufuatlia hali ya mazao na pia kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku.
- **Malisho na upatikanaji wa maji kwa wafugaji:** Wafugaji wanashauriwa kupanda majani ya malisho na kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.
- **Wavuvi wa Samaki baharini na maziwa makuu:** Wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku ili kujua wakati sahihi wa kufanya shughuli za uvuvi kutokana na uwezekano wa kujitokeza mawimbi makubwa na upepo mkali

Ushauri huu umedhamiria kuongeza tija kwenye kilimo na kupunguza athari zitokanazo na hali mbaya ya Hewa. Wadau wote wa kilimo wanahimizwa kufuatilia taarifa za hali ya hewa ili kuwa na mipango thabiti ya shughuli za kilimo.

## HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 1-10, 2026

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuongezeka kidogo hususan katika maneo yanayopata mvua za msimu. Jamii inashauriwa kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo Kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz; agromet@meteo.go.tz; Tovuti: *www.meteo.go.tz*
(ISO 9001:2015 Certified in Aviation Services)